KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

AL-HUDAA [UONGOFU]

الهدى

25/= Ksh

Volume 25, Issue 2

12th Dhul-Qa'dah 1433

28th Sept, 2012

WASILIANA NASI

SIMU (+254) 721473181
Mombasa, Kenya
E-MAIL Info@qssea.net
Web Site: http://www.qssea.net

YALIYOMO KATIKA JARIDA LA WIKI HII

SALAFIYYAH HAINA ... 1 - 3

... MAITI ... 4

HABARI ZA MAZINGIRA YA WAISLAMU KWA MUKHTASAR

Vyama visokuwa vya dini vyaongoza Libya

Ishara za awali za matokeo ya uchaguzi wa mwanzo wa taifa kufanywa Libya kwa karibu nusu karne, zinaonesha kuwa muungano wa vyama visivokuwa vya kidini, unaongoza kwenye majimbo muhimu, pamoja na Tripoli na Benghazi.

Afisa wa daraja ya juu katika muungano wa vyama, uitwao National Forces Alliance, alisema ripoti za awali zinaonesha kuwa wao wanaongoza katika uchaguzi huo uliofanywa Jumamosi, kauli ambayo imethibitishwa na kiongozi mmoja wa chama kinachowapinga, cha Islamist Justice.

Maafisa wa uchaguzi wanasema, matokeo rasmi hayatajulikana kwa siku kadha.

Kati ya viti 200 vya bunge, vyama vya siasa vitapata viti 80 tu. Vilivyobaki vitakuwa vya wajumbe wanaojitegemea. **[BBC London]**

SALAFIYYA HAINA UHUSIANO WOWOTE NA HAO WENYE KUJITA 'SALAFI-JIHADI'

Na: Shaykh Mash-hur Hasan Aal-Salmaan.

"... SISI TUNAPINGA VIKALI MATAMSHI KAMA VILE "SALAFI-JIHADI" NA "SALAFI-TAKFIRI". SALAFIYYAH NI MOJA, NAO NI MFUMO WENYE MKURUBA ULIOEGEMEZWA JUU YA UFAHAMU. AMA KUHUSU VYOMBO VYA UTANGAZAJI VISIVYO NA UWEZO WA KUPAMBANUA, BASI SISI TUNAWASISITIZA KWA UZITO MKUBWA WAJARIBU KUPAMBA-NUA BAINA YA MAS'ALA ..."

Salafiyyah hairudi nyuma, bali Salafiyyah ni mfumo ulio bayana na ni wenye kujifungamanisha vilivyo na wahyi ulioeremshwa wa kisheriya, pamoja na masharuti ya Wanavyuoni wenye kustahiki kusadikika na kuwafanya wao kuwa ndiwo mahakimu na vigezo, kwenye mas'ala makubwa na madogo, katika nyanja zote za maisha ya mtu, wakiyazingatia maneno ya Allaah: **"NA KAMA MKIKHITILAFIANA JUU YA JAMBO LOLOTE BASI LIRUDISHENI KWA ALLAAH NA MTUME."** [An-Nisaa' (4):59]

Katika aya hii 'Shayy' [kitu chochote] ni *'nakira'* [kitu kisichokuwa na mipaka] na *'In'* ni *'Shart'* [ibara ya kushurutisha] na *'nakira'* [kitu kisichokuwa na mipaka] pamoja na *Shart* inaashiriya kwa ujumla. Kwahivyo, iwapo mutazozana kwa lolote, bila ya kujali jambo hilo ni lipi, kwani hili ni kwa ujumla na linahusu jambo lolote. **"NA KAMA MKIKHITILAFIANA JUU YA JAMBO LOLOTE BASI LIRUDISHENI KWA ALLAAH NA MTUME."** [An-Nisaa' (4):59]

Imaam ash-Shafi amesema 'akikusudia 'Kurudi kwa Allaah': kuregea kwenye Kitaab Chake; na kurudi kwa Mtume: Kuregea kwenye utu wake na nafsi yake na Sunnah zake baada ya kufa kwake. Hii ndiyo Slafiyyah. Salafiyyah ni kubwa kuliko ubinafsi, watu mbalimbali, na hata vikundi, Salafiyyah ni kubwa kuliko *Maraakiz* [Vyuo], Salafiyyah ni kubwa kuliko *Jam'iyyaat* [vyama] na ni kubvwa kuliko *Shuyookh* [Mashekhe]. Salafiyyah ni Dini iliyo swafi ya Allaah ambayo Yeye ndiye aliyeiteremsha kwenye moyo wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Hii ndiyo Salafiyyah ambayo tunayoiamini, kwahivyo iwapo sisi tutakuwa ni wenye kusema, kwa min-ajil ya kujadiliana tu, yakwamba watu wale [ma-*Jihadi* na ma-*Takfiri*] ni ma-*Salafi*, basi watatakikaniwa wahukumiwe kulingana na misingi ya Da'wah ya *Salafiyyah* na kama kwamba wanavyopinga sheriya za Jordan wao wenyewe, haliyakuwa asili yao ni watu wa Jordan, wakiwa na vyeti vyao vya usafiri vya nchi ya Jordan na nambari za usajili wa ki-raiya za nchi ya Jordan, sio kwamba sheriya hizo zinawakataza, lakini hata Da'wah ya Salafiyyah pia inawakataza kwa sababu wanakwenda kinyume na misingi ya Da'wah as-Salafiyyah. **Watu hawa [yaani; ma-Jihadi na ma-Takfiri] wanawashutumu ma-Imaam na ma-'Ulamaa' waliotangulia wa Da'wah as-Salafiyyah pamoja na walio hai miongoni mwao, kwa emma kuwachukulia kuwa wamepotoka au kuwa ni makafiri, sasa watawezaje kuwa ni ma-Salafi?! Kustaajabu hakukomi hapo, lakini sisi tunaishi kwenye zama ambazo ndani yake mbinu za ufahamu ulio swaheeh umepinduliwa na pakawa na mabishano makali juu ya istilahi za matamshi na kwahiyo watu wakadanganywa kwa matamshi na majina. Watu leo, isipokuwa kwa waliorehemewa na Allaah, wamekurubia kupoteza ufahamu wa**

(Endelea kwenye Uk. 2)

(Endelea Kutoka Uk. 1)

ki-uhakika. Kwahivyo, kwa mfano utayasikiya maneno ya wenye akili punguani yakisemwa yakwamba "karatasi hii ni nyeusi-nyeupe" hata kama viwili hivyo haviwezi kuwa pamoja kwa wakati mmoja.

Kwahivyo, pindi itakaposemwa "Salafiyyah-Takfeeriyyah" - basi sifa hizi mbili haziwezi kuja pamoja kattu namna hiyo! Hii ni kwa sababu Salafiyyah haikuegemezwa juu ya kufuata mapendelewa (*hawaa*) ya moyo au takfeer, ikiwa hakutopatikana ushahidi ulio dhahiri ambapo tukapata dalili ya wazi kutoka kwa Allaah, basi hairuhusiwi juu yetu kumkufurisha mtu yoyote. Msingi ni kwa Muislamu abakie juu ya hali yake ya asili ya Uislamu, isipokuwa iwapo atadhihirika waziwazi yakwamba anaupinga Uislamu, isipokuwa hivyo, basi atabakia kwenye Dini ya Uislamu.

Mola wetu ametufundisha kutokamana na njia Zake za kuamiliana kilimwengu na viumbe vyake, kwa kutegemea juu ya Matakwa Yake. Wakati wa zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kisa kilichotokea na Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم) akatufundisha msingi muhimu katika suala la takfeer. Wakati ambapo Usaamah ibn Zayd, mwanae kipenzi cha Mtume (رضي الله عنه), alipokuwa kwenye uwanja wa vita, mpiganaji adui alishindwa nguvu na Usaamah na Usaamah akamlemeza upanga kwenye shingo yake ili apate kumuuwa. Yule adui akatamka Shahada: "Mimi nashuhudia yakwamba hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah" na wala Usaamah hakufanya wasiwasi wowote kwa yule adui kuyasema hayo na akamuuwa hivyohivyo. Habari zilipomfikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikasirishwa sana na jambo hilo, Usaamah akamwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Alisema hivyo alipouona upanga tu." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: *"Kwani wewe uliufungua moyo wake?"* Usaamah akasema: "Nilitamani niwe ni mwenye kusilimu kuanzia wakati huo."

Kwahiyo, wanavyuoni wanasema yakwamba iwapo mtu akisema kitu au akifanya kitendo kiwezacho kuzuiya njia mia moja za uwezekano, ikawa njia tisiini na tisa zina uwezekano wa ukafiri, basi inatupasa kuuzingatia Uislamu wake. *Ma-Salafi* ndiwo wachaji Mungu zaidi miongoni mwa watu yanapokuja mas'ala ya takfeer, kwahivyo, hizi ni tuhuma za zamani [yakwamba *ma-Salafi* wanakufurisha watu] na pindi Sheikh wetu (Imaam al-Albaani) alipowasili nchini Jordan kwa mara ya kwanza baadhi ya *mashekhe* wa nchini humo walionana nae na wakamwambia: "Wewe kazi yako ni kuwakufurisha watu!" Sheikh akawajibu: "Naomba hifadha kutoka kwa Allaah!" Kisha Sheikh akamuuliza mmoja wao, ambae ndiye aliyekuja akawa ni mufti wa Jordan baadae na sisi twataraji yakwamba msimamo wake ni mzuri na wenye uadilifu na Allaah atamuuliza kuhusu majukumu yake, "ukimsikiya mtu anayeswali swala ya Sunnah ya Dhuhr akisema 'Nitaziswali kwa ajili ya Mtume', utasemaji kuhusu jambo hilo?" Yule mwanachuoni akamjibu: "Huyo atakuwa ni kafiri". Sheikh akasema: "Ama mimi sitomkufurisha, mtu kama huyo ni mjinga kwahivyo mimi nitamfundisha."

Jambo la kushangaza ni kwamba, watu hao waitwao "*ma-Salafi*", kumbe bado wangali ni *ma-takfeer*, na matamshi hayo mawili hayawezi kuwa pamoja, wakamwita Sheikh wetu, al-Albaani, kuwa ni "*Murji*" na tunapowauliza ni kwanini wanasema hivyo, "ni kwa sababu hakuwakufurisha makafiri na wala hamkufurishi mtu yoyote. Sasa watu kama hao watakuwaje ni *ma-Salafi*?! Ma-Salafi ni watu wenye kumbukumbu za kitaaluma, lakini lau utawauliza wale [wenye kukufurisha watu wanaojiita *ma-Salafi-Jihadi*], "Ni zipi kumbukumbu zenu na 'ilmu zenu munachukuwa kutoka wapi?, basi hapo ndipo utakapogundua yakwamba baadhi yao huwakufurisha *ma-Imaam* wetu.

Kisha, hili neno "Salafi-Jihadi", Jihaad ni mafunzo yapatikanayo kwenye 'ilmu ya Fiqh na yana hukmu zake zinazopatikana ndani ya vitabu na yakatajwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), na sisi kama *ma-Salafi* tunaamini maandiko na matumizi yake. Vilevile, sisi tunaamini yakwamba Jihaad ipo, ambayo tuliyopashwa habari zake na Mtume (صلى الله عليه وسلم), na tunasema yakwamba kupigana Jihaad kwa njia ya Allaah hairuhusiwi kulingana na sheriya iliyoteremshwa isipokuwa kupatikane masharuti matatu, na sisi sio wenye kuyaweka masharuti hayo wala hayakuchukuliwa kutokamana na maoni yetu, bali ni yenye kutokamana na maneno ya Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم). Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah, kutoka katika hadeeth ipatikanayo kwenye swaheeh mbili, yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Imaam ni Ngao na hupiganwa nyuma yake."*

Kwahivyo, kwa kutegemea maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kupigana bila ya kuwa na Imaam [kiongozi] ni jambo ambalo halikuwekwa kisheriya.

Sharuti la pili ni kwamba, bendera iliyoteremshwa ki-sheriya kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) inasema, *"Yoyote mwenye kupigana na akafa chini ya bendera ya upofu [upofu mkaidi] atakufa kifo cha ki-Jaahiliyyah."*

Sharuti la tatu ni: Kuwa Tayari. Hizi ndizo sharuti tatu za Jihaad kwenye njia ya Allaah.

Ama kwa kila mjinga na yoyote anayefanana naye, mwenye kubeba bunduki au upanga na huku akisema, **"Mimi nataka kupigana Jihaad katika njia ya Allaah"**, basi hii si Jihaad kwani kunatakiwa kuwe na matayarisho, ma-Ofisa wa kijeshi, kiongozi, bendera ya ki-Taifa ambayo tutakayopigana chini yake, kwa lengo la kuinua juu neno la Allaah - basi hiyo ndiyo Jihaad tuliyo na Imani nayo. Si kila anayeshika silaha akasema "Mimi nataka kupigana Jihaad" Jee, sisi tunasema yakwamba hiyo ndiyo Jihaad ya kisheriya na katika njia ya Allaah?

Jihaad ni hukmu ya ki-Fiqh yenye sheriya na masharti yake ambayo sisi pamoja na Sheikh wetu tunawalinganiya watu na ambayo tuliyoitilia mikazo kwa kalamu zetu na ndimi zetu, na tukaitaja mahali chungu nzima.

Kwa kumalizia, Salafiyyah ni njia ya mfumo kamili, kanuni za Imani na utaratibu wa ki-Ilimu katika ulinganizi unaoamini kuwatwi'i viongozi na kukataza kuwa'asi au kujiondoa kwenye twa'a yao. Vilevile, Salafiyyah inaamini kuwepo kwa Jihaad kuwa ndicho kinara cha Uislamu na kuwa ni Hukmu ya Allaah ili isipate kutumiwa kwa njia ambayo ni mojawapo ya utani unaoweza kuleta madhara katika usalama wa nchi, huo ni uhalifu wa Sheriya ya Mungu, Dini (ya Uislamu), na Da'wah iliyobarikiwa.

Kuna njama nyingi sana zinazofanywa dhidi ya Da'wah hii iliyobarikiwa, wakiwemo walio hatari zaidi ni wale ambao sio miongoni mwa Da'wah waliojivisha mavazi yake. Kwahiyo kumekuwa na juhudi kubwa sana kutoka kwa Wanavyuoni wetu katika kukabiliana na haya kwa kuwabainisha watu sampuli hiyo na mifumo yao ya ufisadi. Njama hizi hujirudia upya mara kwa mara,

kwahivyo ni wajibu juu ya vijana wa Da'wah hii wajitenge nao na wasimame wima katika kubainisha Dini ya Allaah. Da'wah ya Salafiyyah si Da'wah ya Siyasa, ni Da'wah ya usalama, 'ilmu, mfumo wa kuifahamu Dini ya Allaah, ta'luma na vitendo - Hii ndiyo Da'wah ya Salafi, si U-hizbiyyah. Yoyote mwenye Imani iliyo swaheeh ya Uislamu ni Salafi maana yake: Anakitukuza Kitabu cha Allaah, Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم), Maswahaba, waliowafuata na waliowafuata hao - yoyote mwenye kuafiki haya ni Salafi.

Sisi hatuna Da'wah iliyojengwa juu ya U-hizbiyyah na U-majimbo, hatahivyo, hatuwataki hao waje kwenye swafu zetu na wale wasiotokamana na Da'wah hiyo, walioshikilia rai zao za ubinafsi zenye kutupinga sisi na kuisambaratisha Da'wah yetu kutokana na udanganyifu huu. Watu hawa hawaifahamu Dini jinsi tunavyoifahamu sisi na hawaregei nyuma kwa Wanavyuoni ambao sisi tunaowaregelea kwao, na hawaizingatii misingi tuliyoshikamana nayo yaliyoegemezwa juu ya Kitaab cha Mola wetu na Sunnah za Mtume wetu.

Tunawashukuru wale wote wenye kutafautisha baina ya Da'wah ya [Salafi] na isiyokuwa hiyo na kunakataa majina kama vile "Salafi-Jihadi" na "Salafi-Takfiri".

Salafiyyah ni moja. Ni mtizamo wa mfumo uliojengwa juu ya ufahamu. Ama kuhusu vyombo vya utangazaji visivyo na uwezo wa kupambanua, basi sisi tunawasisitiza kwa uzito mkubwa wajaribu kupambanua baina ya mas'ala na watangaze yakwamba sisi hatuhusiani na vitendo vya sampuli hiyo na mas'ala yetu na hao [wenye kuwakufurisha watu] ni ya kale na si mambo ya mzaha. Sisi hatuwaoni kwenye mikao yetu wala hatusikii lolote kuwahusu wao isipokuwa tu wao wanatuchukulia sisi kuwa ni watu wapotofu pamoja na mashekhe wetu na ndugu zetu miongoni mwa mashekhe.

Wao si miongoni mwetu na wala sisi si miongoni mwao vilevile katika vitendo vyao au katika ufahamu walio nao.

Salafiyyah haikujengeka juu ya U-Hizbiyyah au ubinafsi, shughuli zetu ni kuwafundisha watu tu "Amesema Allaah", "Amesema Mtume wa Allaah" na "Wamesema Maswahaba". Sisi tunaamini yakwamba Umoja ndio wenye kusababisha kupata nguvu katika Ummah na sababu za nguvu zinatokana na Wanavyuoni pamoja na viongozi, kama alivyoeleza Sufyaan ath-Thawree: **"Watu sampuli mbili, iwapo watarekebishwa basi watu wote watarekebishika na lau watafisidika basi watu wote watafisidika: viongozi na wanavyuoni."** Sababu za Ummah kupata nguvu kwahivyo, ni lazima zipatikane na kuletwa kwa pamoja pasi na kutenganishwa, hivi ndivyo tuonavyo sisi. ma-'Ulamaa waliwaombea Mungu ma-'Umaraa' na wakamuomba Allaah awaja'aliye kufuzu kama alivyosema Fudhayl Ibn 'Iyyaad: "Lau kama ningelikuwa na nafasi ya kuomba *Du'a'a* moja tu itakayojibiwa, basi ningelimuombea kiongozi. Kwa sababu kwa kurekebishika kwake ndiko kurekebishika kwa watu, na kwa uharibifu wake ndio uharibifu wa watu.

Vilevile kwa wenye kutoa khutba (ma-Khutwabaa'), wanafunzi wa ki'ilimu, wahubiri na wenye kuwalingania watu kwenye Dini ni wanajeshi wa *ma-'Ulamaa'* uhusiano baina yao ni lazima utegemezwe juu ya kuheshimiana kila mmoja katika nyadhifa walizonazo baina yao na wala wasitegemee juu ya ubinafsi, na kama hivyo ndivyo inavyowajibika kwa uhusiano baina ya wanavyuoni (*ma-'Ulamaa'*) na viongozi (*ma-Umaraa'*).

Ma-'Ulamaa hutoa *naswaha*, wakaamrisha na wakakataza kwa *hikmah*, wakawa na maneno mazuri na kuwa na ulinganizi mzuri kama walivyokuwa wakifanya *ma-Salaf*.

THE QUR'AN & SUNNAH HAJJ / 'UMRAH AGENCY

1433 HIJRI/ 2012 C.E

Assalaamu 'Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah Barnaamij yetu ya mwaka huu 1433 Hijri/ 2012 ya Hajj.

Mipangilio Ya Safari

- Kuondoka ni katika wiki ya mwisho ya mwezi wa Dhul Qa'dah
- Kurudi ni mwisho wa mwezi wa Dhul-Hijjah
- Safari itaanza Mombasa – Nairobi – Jeddah
- Kurudi ni Jeddah – Nairobi – Mombasa
- Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli, Usafiri na Chakula – mara 3 kwa siku tukiwa Mina kwa siku tano)
- Class "C" ni $3300 U.S Dollars
- Tutakuwa na Darsa juu ya mas'ala ya Hajj kabla ya kuondoka na tutakapokuwa Makkah

Kwa Maelezo Zaidi

Fika katika Maktaba ya QSS iliyoko ubavuni mwa Tajj Hotel (Duka la tatu baada ya Duka la vitabu vya Dini), au

Wasiliana nasi kwa kutuandikia barua Pepe kwa info@qssea.net, au

Tupigie simu nambari mojawapo ya hizi zifuatazo:

+254 723471820 au +254 721473181, au +254 700365253

MAMBO YENYE KUMFAA MAITI

Abu Ameenah Bilaal Philips (حفظه الله)

Qur'an imesimamisha mambo mawili ya furugh (kwa ujumla) kuhusu malipo na adhabu kwa matendo:
Kila mwana Adamu kwa msingi atanufaishwa au kudhuriwa na matendo ambayo yeye ameyatenda. **Allaah** asema: [**Na kwamba mtu hatapata ila yale aliyo yafanya-AN-NAJM 53:39]**
Hakuna mtu atakaye beba madhambi ya mwengine. **Allaah** asema: **[kwamba haichukui nafsi dhambi za nafsi nyingine-AN-NAJM 53:38]**
Hivyo basi mtu atakapo kufa, fursa yake yakutenda mema itakuwa imekwisha kwa kufa kwake. Lakini fursa ya kuvuna mazuri kutokana na matendo yalio fanywa kabla ya kufa kwake yabakia.
DU'AA –maombi ya Waislamu kwa niaba ya aliyekufa yatamnufaisha maiti, kwa ruhusa ya **Allaah.** Ikiwa hawakufanya mema hakuna ambaye angeshughulika kuwaombea. Ikiwa walikuwa waovu, maobi ya wengine hayawanufaishi.
Allaah awasifu waumini wanao waombea wenzao walio tangulia kabla ya wao: **[Na (kadhalika wapewe mali hayo Waislamu) waliokuja baada yao (wakawa wanapendana na Waislamu walio tangulia, wanawaombea dua) wanasema: "Mola wetu tusamehe sisi na ndugu zetu walio tutangulia (kufa) katika Uislamu. Wala usijaalie katika nyonyo zetu undani kuwafanyia Waislamu (wenzetu). Mola wetu! Hakika Wewe ni Mpole sana. Mwenye rehema mno."-AL-HASHR 59:10]**
Zaidi , swala ya jeneza yenyewe inayo ndani yake haswa maombi kwa maiti.
Safwan [rawi alitaja kuwa Safwan ibn Abdillah ibn Safwan(رضي الله عنه)) alikuwa amemuoa ad-Dardaa] alisema: "nilimzuru Abud-Dardaa (رضي الله عنه) nyumbani kwake Syria, lakini sikumuona yeye humo. Ummud-Dardaa' (رضي الله عنها) akaniuliza 'utakwenda kufanya Hajj mwaka huu? Nikasema 'Naam' akasema: 'tuombee kwa Allaah mema kwetu, kwani Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "maombi ya Muislamu kwa nduguye akiwa mbali (absent) hayuko, yatajibiwa. Maadamu amuombea nguguye mema, kuna malaika aliye pewa jukumu lakuwa karibu yakichwachake anaye sema: Ameen, na pia wewe upate kama hayo.'
Nikaondoka nikaeda sokoni ambapo nikakutana na Abud-Dardaa' na yeye akanihadithia hayo hayo kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) swaheeh Muslim vol.4 p.1429, no.6590]
SAUMU- Funga zilizo kusekana na maiti aweza kufungiwa kwa niaba yake na walio karibu naye. Na funga zaweza kuwa ni za ramadhan au nadhiri
Aa'ishah (رضي الله عنها) alihadithia kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) akisema: "Yeyote atakaye kufa akidaiwa saumu, mwangalizi wake naafunge kwa niaba yake" [sahih Al-Bukhaari, vol. 3, p.99 #173 na sahih Muslim, vol. 2, p.# 2553]
Ibn Abbaas (رضي الله عنه) alisema "Mtu alikuja kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) akauliza 'Ya Rasula Allaah, mama yangu alikufa akiwa adaiwa mwezi mmoja wa saumu. Ni mfungie kwa niaba yake? Akamjibu (صلي الله عليه وسلم): "Naam, deni za Allaah alihaki zaidi ya kulipwa." [Sahih Al-Bukhaari, vol.3, p.99, no. 174, na Sahih Muslim, vol.2,p.556, #2554] katika riwaya nyingine mwanamke aliuliza kuhusu deni la mama yake la saumu na akapawa jibu kama hilo. [Sahih Muslim, vol, 2, pp.556-7, nos. 2554, 2557-61]
KULIPA MADENI YA MALI- Yeyote aweza kumlipia aliyekufa madeni yanayo ambatana na mali, pesa na kadhalika ikiwa ni walio na uhusiano naye au la. Mbali na hayo kulipa madeni ya maiti yaweza kumnufaisha yeye kupunguziwa baadhi ya adhabu kwa sababu ya kudharau kulipa madeni hayo.
Jaabir (رضي الله عنه) alisema: mtu alikufa na tukamuosha, tukamtia manukato, na kumvalisha sanda. Kisha tukamleta kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) ili atuongoze katika kumswalia swala ya jeneza. Tukamuulza waweza kumswalia? Akichukuwa hatuwa mbele kisha akauliza, 'Anayo madeni anayo daiwa? Tukamjibu, 'Deenar mbili.' Akasema, "mswalieni swahib wenu' na [nyongeza hii yaweza kupatikana katika hadeethi nyingine] akaanza kuondoka' Aboo Qataadah (رضي الله عنه) akachukuwa jukumu lakulipa deni hilo, alisema "deenari mbili ni jukumu langu' Mtume (صلي الله عليه وسلم) akauliza, "Anaye dai ataangaliwa (kulipwa) na maiti ataondokewa na deni? Akajibu 'Naam' kwa hivyo Mtume (صلي الله عليه وسلم) akaswalisha swala ya jeneza. Siku moja baadaye akauliza [Aboo Qataadah] mlifanya nini kuhusu deenar mbili? Akajibu ' amekufa jana tu! Siku ilio fuatia akarudi kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) akasema, nimelipa, Mtume (صلي الله عليه وسلم) akasema, sasa ngozi yake imepoa moto" [Musnad Ahmad vol.3, p.330' imeswahihishwa katika Ahkaamul-Janaa'iz p.16]
SWADAKA YA WATOTO –wazazi watanufaika kutoka na matendo yoyote mema watoto wao wanayo yafanya bila ya kuwapunguzia ujira wao (watoto). Mtoto mwema azangatiwa kuwa katika mapato ya wazazi.
'Khalati yake Umaarah ibn 'Umayr (رضي الله عنهم) alimuuliza Aa'ishah (رضي الله عنها), "nina yatima chini ya ungalizi wangu. Naweza kula baadhi ya mali yake? Akajibu (Aa'isha) kuwa alimsikia Mtume (صلي الله عليه وسلم) akisema: "Kati ya miongoni mwa vitu vyenye kufurahisha ni mtu kula katika mapato yake, na mwanawe ni katika mapato yake." [Sunan Abu Daawood vol. 2, p.1002,=no.3521. ikaswahihishwa katika sahih Sunan Abu Dawood vol. 2, p. 674, no. 3013]
Aaishah رضي الله عنهاalihadithia kuwa mtu alimuuliza Mtume (صلي الله عليه وسلم): "Mama yangu amekufa ghafla, na nafikiri kuwa ikiwa angeliweza kuzungumza (kabla ya kufa) angelitoa kitu kwa sadaka. Nikitoa mimi sadaka kwa niaba yake, atapata ajri? Akajibu, 'Naam" [Sahih Al-Bukhari vol. 2 p.266, no.470, sahih Muslim, vol. 3 p.866, no.4002, na Sunan Abu Daawud, vol. 2. P.812, no. 2875]
Aboo Hurayrah (رضي الله عنه) alihadithia kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم): "Mtu akifa , matendo yake yakatika (ya mwisho), isipokuwa katika hali tatu: sadaka inayoendelea, ilmu ambayo watu waendelea kunafaika nayo, na mtoto mwema anaye kuombea." [Sahih Muslim, vol.3,867, no.4005, na Sunan Abu Daawud, vol.2, p.812, no.2874]

MWENYE KUJI-PAMBA NA SIFA AM-BAYO SI YAKE HUFEDHEHEKA WA-KATI WA MITIHANI.

-Salaf.